

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Anuani ya Simu: "TAMISEMI"
Simu Na: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420
Nukushi: (026) 2322116,
2322146,2321013
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa,
S.L.P. 1923,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Yah: KUSITISHWA KWA MUDA KWA ZOEZI LA UHAMISHO

Itakumbukwa kwamba katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(OR-TAMISEMI) imefanya uhamisho kwa baadhi ya watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa .

Baada ya kufanyika kwa uhamisho huo imeonekana kuwa ipo haja ya kufanya tathmini ya kina juu ya namna zoezi la uhamisho linavyofanyika ili kuweza kuboresha zaidi utoaji wa huduma hiyo. Sambamba na tathmini hiyo, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora zipo katika hatua za kutengeneza mfumo wa kieletroniki wa maombi ya uhamisho ili kuwawezesha watumishi waliopo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupata huduma za uhamisho kwa haraka na urahisi zaidi.

Kwa mantiki hiyo, tunapenda kuwataarifu watumishi wote waliopo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa zoezi la uhamisho wa Watumishi kutoka katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa limesitishwa kwa muda hadi hapo tathmini ya kina ya utoaji wa huduma hiyo itakapokamilika.

Baada ya zoezi la tathmini kukamilika, mtajulishwa kuendelea kwa zoezi hili kupitia tovuti rasmi ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na mitandao yake ya kijamii ambayo ni. (www.tamisemi.go.tz)

Imetolewa na:

Rebecca Kwandu
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
Ofisi ya Rais,
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
28Agosti, 2018.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

1.0. UTANGULIZI

Tarehe 09 Desemba, 2015 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli aliagiza Maadhimisho ya sherehe za Uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutumika katika kufanya kazi. Katika agizo hilo Mhe. Rais aliwataka Watanzania kuitumia siku hiyo kama kichocheo cha kujenga tabia ya kufanya kazi na kutimiza dhana ya uhuru ni kazi. Katika siku hiyo Mhe. Rais alitumia siku hiyo kuwaongoza Watanzania kufanya usafi wa mazingira katika eneo la Feri Jijini Dar es Salaam.

2.0. NAMNA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA INAVYOTEKELEZA ZOEZI LA USAFI WA MAZINGIRA NA KULIFANYA ZOEZI LA USAFI ENDELEVU.

Katika kuhakikisha kwamba zoezi la usafi na mazingira linakuwa endelevu, Ofisi ya Rais TAMISEMI ambayo ndiye msimamizi mkuu kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa imeamua kuanzisha utaratibu wa ukaguzi wa usafi na mazingira katika mikoa yote nchini.

Ukaguzi huo umepangwa kufanyika katika maeneo mbalimbali kama maeneo yote ya masoko, nyumba za kulala wageni, Migahawa na Mahoteli, Maeneo ya Baa na Minada, makazi wa wananchi, maeneo ya barabara, mifereji ya maji ya mvua na maji taka na sehemu zilizotengwa wazi ambapo Makatibu Tawala wote nchini wameagizwa kusimamia zoezi hilo kwa mwongozo utakaotolewa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Pamoja na kufanya uhakiki na ufuatiliaji wa shughuli za usafi na mazingira Ofisi ya Rais-TAMISEMI pia inazijengea uwezo timu

za kiufundi na kiutawala za Mkoa na kutembelea hospitali za rufaa Mkoa na za taasisi za Dini/Binafsi.

Aidha, katika zoezi hilo la uhakiki Ofisi ya Rais TAMISEMI inaziwezesha timu za kiufundi za wilaya/halmashauri na kutembelea hospitali ya wilaya.

Pia katika zoezi hilo Ofisi ya Rais TAMISEMI inaziwezesha timu za wilaya/halmashauri kuzijengea uwezo timu za hospitali/vituo vya afya, zahanati na jamii na kutembelea hospitali na vituo vya afya, zahanati na jamii.